## Mgawanyo wa fedha

Fedha iliyotengewa wizara ya ustawi wa uvuvi ni ndogo mno ikilinganishwa na wizara nyingine, ilhali viwango vya umaskini viko juu sana miongoni mwa wavuvi wa pwani na wale wa eneo la ziwa.

## Mapendekezo

1. Tungependa kuona kwamba taratibu za BMU(2007) zimechambuliwa tena kuzihakiki na kuzirekebisha ili ziweze kuangazia maswala maalum ya uvuvi wa pwani na bahari.

2. Fedha inayotengwa wizara ya ustawi wa uvuvi kutoka kwa mgawanyo wa kila mwaka ziongezwe. Twaomba wizara kutia mkazo uhusiano kati ya upunguzaji wa umaskini na utawala na usimamizi bora wa uvuvi. Inabidi serikali iwezeke katika sekta hii kuambatana na kielelezo cha sera ya uvuvi inayoundwa bado.

3. Tungependa ardhi ya umma yote ufuoni iliyoingiliwa na kumilikiwa kwa njia ya haramu ibatilishwe, ipimwe na hati miliki iwe chini ya ulinzi wa idara ya uvuvi kwa minajili ya matumizi ya umma.

4. Mtandao wa ushirika wa kitaifa wa uvuvi wa pwani uundwe na kuzatitiwa ili wavuvi wawe na sauti na uwakilishi hasa kwenye kamati zinazoteuliwa na serikali kuchunguza, kuhakiki na kubuni sera na taratibu.



Ofisi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafiti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendelevu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa "uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki" unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafiti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

Maoni yaliyotolewa kwa chapisho hili si lazima kuwa mawazo ya mitizamo ya IUCN, IDRC, The Ford Foundation, KNCF, CORDIO au EAWLS.

Sifa kwa picha: Nyaga Kanyange/CORDIO
P. Gichuhi/EAWLS
H. Becha/EAWLS

IUCN IDRC CRDI
KNCF CORDIO East Africa THE EAST AFRICAN WILD LIFE SOCIETY

# Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Kenya



# BMUs

## (Usimamizi Tawala wa Kitengo cha Ufukwe)

Na:
Fatuma Musa
Said Ali Chufu
Hamis Juma
Norman Sulubu
Pendo Morris Charo
Emmanuel Yaa

# Utangulizi

Ilani ya kisheria nambari 402 ya sheria ya uvuvi (sura 378) ina taratibu ya uvuvi(usimamizi tawala wa vitengo vya ufukwe-BMUs) 2007. Taratibu hizo zimeandaa njia ya kuzatiti BMU kwa kila bandari ya uvuvi katika pwani.

Shabaha za BMU miongoni mwa nyingine:

- Anzisha maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi.
- Saidia kupunguza umaskini na kuboresha ustawi na chuma riziki kwa wanachama kwa njia ya utawala bora na demokrasia, mpango wa usimamizi bora wa rasilimali na kujitegemea.
- Imarisha usimamizi wa bandari za samaki, rasilimali na kujitegemea.
- Tambua majukumu ya wadau mbalimbali wa sekta ya uvuvi, wakiwemo wanawake.
- Zuia au punguza migongano ndani ya sekta ya uvuvi.

Utawala wa BMU huwa na muundo ufuatao. Kongamano la wanachama, kamati ya utendaji na kamati ndogo ndogo. Uanachama wa BMU uko wazi kwa mtu yeyote anaetegemea uvuvi na ufukwe kwa mapato ya kifedha au kujikimu maisha. BMU inaruhusiwa kutunga sheria zake ndogo ndogo.

Eneo la mamlaka ya BMU ni bandari ya uvuvi iliyotengwa kwa ajili ya kutuwisha na kuuza samaki na bidhaa za samaki. BMU inatakikana kuhakikisha usalama, ustahiki na usimamizi bora wa bandari. Inaweza kuwahamasisha na kuwapa mafunzo wanachama wake, kama vile mbinu za kuvua, mauzo, utayarishaji wa samaki, usimamizi wa fedha. BMU pia huwezesha vikundi binafsi vya wavuvi vya ushirika na kujisaidia.

Kila mwanachama wa BMU ana majukumu maalum, ikiwemo kupiga doria. Mwaka 2007 BMU kadhaa zilianzishwa katika pwani ya Kenya. Hizi ni pamoja na Lamu, Kipini, Gongoni, Ngomeni, Bamburi na Mida.

Warsha ya kitaifa ya jamii ya pwani ilifanyika Kilifi kuanzia tarehe 17 hadi 19 Disemba 2008. Lengo la warsha lilikuwa kuzipa jamii za pwani fursa ya kutangamana na kubadilishana uzoefu wa usimamizi na utendaji kwenye rasilimali za baharini pamoja na kuelezea kwa ufasaha mahitaji yao. Kama wakilishi wa BMU sita, tulitoa maoni yetu, malengo, shughuli, masuala nyeti na mapendekezo katika mkutano huo.

# Muhtasari wa malengo, shughuli na maswala nyeti

| JINA LA BMU | LENGO NA SHUGHULI | MASWALA NYETI |
|---|---|---|
| Takaungu<br>Kilifi | • Kuwaleta pamoja wadau wote wa Takaungu<br>• Uvuvi endelevu<br>• Uhifadhi wa mazingira k.m upanzi wa mikoko | • Uchafuzi wa taka kutoka kiwanda cha mkonge cha Vipingo<br>• Ukosefu wa vifaa na ujuzi wa uvuvi<br>• Umiliki haramu wa bandari za uvuvi na mabepari waendelezaji binafsi |
| Gongoni<br>Malindi | • Uregeshaji hali bora ya mikoko | • Ukokooro kwenye ghuba ya Ungwana<br>• Uharibifu wa mikoko kutoka kwa mashamba ya chumvi |
| Ozi<br>Mto Tana | • Uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili<br>• Kupunguza umasikini | • Ukandamizaji wa wavuvi wadogo wadogo na wafanyabi-ashara kubwa wa samaki<br>• Idara ya uvuvi kutowajibika kudhibiti sheria ya uvuvi. |
| Mida<br>Malindi | • Usafishaji wa ufuko<br>• Uregeshaji wa mikoko<br>• Kuwabandika kasa vibandiko | • Uchafuzi wa kutoka kwa taka za matibabu<br>• Mgongano kati ya watumiaji Wa rasilimali ya bahari(km kati ya wavuvi na wenye mashua, kati ya wavuvi, wenye hoteli na KWS) |
| Bamburi<br>Mombasa | • Hamasisha juu ya uhifadhi<br>• Kujifunza na kuiga mbinu za kisasa za uvuvi<br>• Kupanua matumizi mbali mbali ya rasilimali ili kuzidisha mapato ya fedha. | • Ukosefu wa vifaa bora vya uvuvi<br>• Ukosefu wa kituo cha mafunzo cha kuelimisha na ku-hamasisha wanachama |
| Amu<br>Lamu | • Uvuvi endelevu | • Ukosefu wa zana bora za uvuvi |

# Maswala nyeti

## Umiliki wa ufuoni (fukwe) na ardhi

Ardhi ya umma ufuoni mwa bahari imeingiliwa kiholela na waendelezaji wa kibinafsi au mabepari na imetaliwa kwa njia isiyo halali. Jambo hili limezidishwa nguvu kutokona na mgongano wa sheria mbalimbali kuhusu umiliki wa ardhi hizi. Kwa mfano, sheria ya wanyama pori imetenga kipimo cha mita 30 kutoka ufuko. Ile ya upimaji ardhi (survey) kwa upande mwingine imeweka kiwango cha mita 60. Matokeo na athari yake ni shida inayokumba umma kupata njia ya urahisi kufika au kuingia ufuoni. La muhimu, kumezidi kuwa vigumu kwetu sisi kupata fursa ya kutumia bahari na fukwe kwa masilahi ya kuchuma riziki.

Bandari za kutua samaki pia zimemilikiwa kwa njia isiyo halali. Hatuna uhakika ni bandari ngapi zimeorodheshwa na kutambuliwa rasmi na idara ya uvuvi, wala hatuelewi sababu za idara ya uvuvi kutoweza kubatilisha umiliki huu haramu.

Mgongano baina ya jamii ya wavuvi wa kawaida na waendelezaji wa kibinafsi husussan imejitokeza Diani, Shanzu, Bamburi, Watamu na Malindi. Ugomvi huu ukijumuishwa na ufisadi umezidisha shida ya kutowajibika na kutodhibiti sheria.

## Sheria ya BMU

Mfumo wa usimamizi wa BMU ni hatua muafaka kwa utawala na usimamizi husishi wa uvuvi. Hata hivyo, sheria hii ilipitishwa mwaka 2007 na ina mianya. Sababu ni kwamba, muundo huu wa BMU umeigwa kutoka uvuvi wa ziwa Victoria. Hivyo basi haujarekebishwa kuwiana vyema na uvuvi wa bahari. Kwa mfano, maeneo ya kuvua samaki ni mamoja kwa uvuvi wa baharini. Mvuvi kutoka BMU yeyote ana uwezo wa kuvua maeneo haya. Kuna uwezekano wa migongano kati ya BMU mbalimbali siku za usoni ikifahamika ya kwamba kila BMU inatakikana kumiliki eneo lake binafsi.

